COUNTY MOCK EXAMS-STD 8
2016

KISWAHILI PAPER

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website:www.schoolsnetkenya.com

SIAYA COUNTY MOCK

DARASA LA NANE - MWAKA 2016

Muda: Saa 1 Dakika 40

SEHEMU YA KWANZA:
KISWAHILI: LUGHA

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina Maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu.

NAMBA YAKO YA MTIHANI
JINA LAKO
JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika kisanduku zenye namba zinazokuhusu. Onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa Herufi. A. B. C. D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Kwa mfano:

Katika kijitabu cha maswali

Tegua kutendawili:-
23. Kutoa ni kuongeza.
A. Handaki
B. Shimo
C. Maji
D. Mavuno

Jibu sahihi ni B (Shimo)
Katika karatasi ya majibu:

23 [A] ~~[B]~~ [C] [D] 24 [A] [B] [C] [D] 25 [A] [B] [C] [D] 26 [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 30, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne uliyopewa.

FUNGUA UKURASA

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 - 15 kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jib tifaalo zaidi ya yale uliyopewa

Safari ____1____ tulikuwa ____2____ safari ya mbali. Wanawake wali ____3____ mizigo kichwani na wanaum wakai ____4____ mabegani. Watoto wadogo wali ____5____ migongoni.

Safari yenyewe ilikuwa ____6____ sana. Tulitembea ____7____ miguu. Baada ya ____8____ mrefu tuliketi chi ya kivuli ____9____ mwanana ulituburudisha. Kina mama waliwa ____10____ watoto wao mapajani kuwanyonyesha Nilikunywa maji kwa pupa ____11____. Nilikohoa mpaka machozi yakanitiririka.

Kulikuwa na joto ____12____ na mizigo ilikuwa mzito kama ____13____. Tulichoka lakini ____14____ na bud kuendelea ____15____ hicho kuliwavutia watu wengi.

1.	A. moja	B. mmoja	C. kimoja	D. mocha
2.	A. tutaenda	B. tulienda	C. tunaenda	D. tukienda
3.	A. pepa	B. twika	C. eleka	D. inua
4.	A. pakata	B. eleka	C. angata	D. twika
5.	A. elekwa	B. angata	C. pakata	D. twika
6.	A. refu	B. kirefu	C. mrefu	D. ndefu
7.	A. za	B. wa	C. kwa	D. na
8.	A. safari	B. mwendo	C. njia	D. kutembea
9.	A. hewa	B. vumbi	C. baridi	D. upepo
10.	A. angata	B. kamata	C. pakata	D. shika
11.	A. nikakamwa	B. nikasakamwa	C. nikapaatwa	D. nikanyongwa
12.	A. jingi	B. nyingi	C. mingi	D. mwingi
13.	A. chumba	B. mawe	C. mizigo	D. nanga
14.	A. hatukua	B. tulikuwa	C. hatukuwa	D. tunakuwa
15.	A. chalo	B. chama	C. charo	D. kikosi

Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi

16. Mfaka mia ni karne ilhali ishirini ni kwa
A. kukuli B. korija C. mwongo D. lukuki

17. Ikiwa leo ni Jumamosi, Jumamosi itakuwa:
A. kisomba B. mtondo C. kitojo D. kitojotojo

18. "KI" imetumikaje katika sentensi?
Mwanafunzi huyo aki kuona atatembea ki jeshi.
A. masharti, namna B. wakati, nomino
C. wakati, namna D. masharti, nomino

19. Ni upi ukubwa na wingi wa sentensi ifuatayo?
Ng'ombe mkubwa limechinjwa
A. Gombe kubwa limechinjwa.
B. Jogombe jikubwa limechinjwa.
C. Magombe makubwa yatachinjwa
D. Majigombe makubwa yamechinjwa.

20. Kamau alienda kumfariji Chege baada ya maziko ya babaye. Alimwamkia makiwa, je, Kamau alijibu:
A. tunayo B. yamepita C. asante D. nishapoa

21. Chagua usemi halisi ulio sahihi wa sentensi ifuatayo:
Zainabu alisema kwamba Ziwa Victoria mna viboko wanono.
A. "Ziwa Victoria mna viboko wanono," Zainabu alisema.
B. Zainabu alisema kwamba, "Ziwa Victoria mna viboko wanono."
C. "Alisema Zainabu, Ziwa Victoria mna viboko wanono."
D. "Zainabu," Mna viboko wanono Ziwa Victoria.

22. Faini ni kwa haka na kuepua ni kwa _____
A. kukuka B. kusonga C. kuinjika D. kudeua

23. Chagua orodha ya nomino pekee.
A. Lima, ua, ota, kabisa
B. Rungu, Juma, Nairobi, Kibukusu
C. Mungu, lewa, kisu, la
D. Lakini, kando, muda, imba

24. Ni sentensi gani iliyo na maana ya:-
Amekuja akalakiwa?
A. Angalikuja angalilakiwa
B. Angekuja asingelakiwa
C. Asingekuja asingelakiwa
D. Asingelikuja asingelilakiwaa

25. M[illegible]a ulipigwa uwanjani. Nyambua katika hali ya kulendeka.
A. Mpira ulipigwa uwanjani
B. Mpira ulipigisha uwanjani.
C. Ulipiliga mpira uwanjani
D. Mpira ulipigika uwanjani

26. Matumizi ya 'kwa' ya pamoja ni:-
A. moja kwa mbili
B. kwa nini hukuja shuleni jana
C. vijana kwa wazee walifika bandarini
D. alienda ng'ambo kwa masomo zaidi

27. Radidisha nomino uliyopewa. Maudhari
A. haya haya B. yaya haya
C. kile ile D. wawa hawa

28. Methali ipi iliyo sawa na ile umepewa?
Mgagga na upwa hali wali mkavu.
A. Bidii ni mali
B. Mchumia janga hula na wa kwao
C. Hamadi kibindoni
D. Dunia ni msufi mkavu

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

29. Taja jina la umbo hili:



A. Nusuduara
B. Kizio
C. Kipenyo
D. Tufe

30. Kifaa kipi hutumika wakati wa mchezo wa rugwe?
A. Upondo
B. Mpira
C. Kikapu
D. Kamba

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kutoka 31-40

S.L.P. 20,
SAUDIA.
5/6/2000

Kwa mwanangu Zaina,

Pokea salamu nyingi kutoka kwangu. Baada ya salamu hizo, ningependa kukuarifu kwamba nimepata barua yako y tarehe 6 - 5 - 2000.

Nafurahi kusikia kuwa umeanza masomo yenu ya kidato cha kwanza. Natumaini utaendelea kusoma kwa bidii kam mwaka jana ulipokuwa darasa la nane. Kumbuka ya kuwa inakubidi utie bidii sana katika masomo yako. Kutii sheria zot za shule na kutangamana vyema na wanafunzi wenzako. Bila shaka wayafahamu haya, maana wewe si mtoto mdogo tena Kwani unaweza kupambanua jema na baya. Lakini inafaa wanadamu kukumbushana.

Katika barua yako umenung'unika kuwa chakula hakiivi sawa sawa. Hapo sikubaliani nawe sababu kuwa kila siku mnakula chakula aina moja. Nafikiri unatia chumvi. Kule kutoiva kwa chakula mara kwa mara si jambo lisilokuwa la kawaida. Hata huku nyumbani, mara nyingi kikipikwa kabisa ama kukosa chumvi ama viungo. Sina mengi zaidi ya hayo Hivi karibuni utapokea pesa kupitia kwa mwalimu wako wa darasa. Nitamtumia kwa njia ya M-pesa. Zitakusaidia kwa masurufu yako.

Pokea salamu kutoka kwa mama yako Sauda na ndugu zako Neema na Baraka. Usikose kutuandikia barua mara kwa mara au kutupigia simu kutujulisha hali yako.

Mpenzi baba yako,

Mwinyi Mumunye.

31. Baba alimwandikia mwanawe barua muhula gani?
A. Wa kwanza
B. Wa tatu
C. Hawajasema
D. Wa pili

32. Mtoto aliyeandikiwa barua na babake
A. alikuwa amecheza na masomo katika darasa la nane
B. hakujitahidi sana katika darasa la nane
C. alikuwa amefanya vibaya katika mtihani wake
D. alikuwa ameupasi mtihani wake wa darasa la nane

33. Zaina amelalamika kuwa chakula cha shule:
A. wakati mwingine hakiivi
B. wakati wote hakiivi
C. hakina viungo
D. hakilikl

34. Neno bidii lina maana sawa na juhudi. neno jingine lenye maana sawa na sheria?
A. Kanuni
B. Mwenendo
C. Kawaida
D. Desturi

35. Babake Zaina _____
A. anakubaliana na malalamishi ya mwanawe
B. anamsuta mwanawe kwa tabia ya kunung'uniko
C. anasadiki kuwa mwanawe hana adabu na bidii
D. anaonelea mwanawe hatii sheria za shule

36. Ni maelezo yapi ambayo si sahihi?
A. Mumunye anatilia mkazo kuwa kusoma ni muhimu
B, Baba anahimiza mwanawe kuwa na adabu daima
C. Baba anamkumbusha mwanawe awe na bidii
D. Mwinyi anamshauri mwanawe awepende wanafunzi pekee

37. Katika barua hii, tunaona chakula kinachopikwa nyumbani:
A. kinapikwa ovyoovyo
B. kawaida hakiongezwi chumvi
C. hakitofautiani sana na cha shuleni
D. hakina viungo na hukosa ladha

38. Kifaa kipi hutuma pesa kwa njia ya M-pesa?
A. Redio
B. Rukono
C. Pataninga
D. Ngamizi

39. Pesa ambazo Zaina ataturniwa ni za kazi gani?
A. Karo
B. Nauli
C. Matumizi
D. Chakula

40. Methali gani kati ya hizi inatoa ufafanuzi wa waraka huu?
A. Mcheza kwao hutuzwa
B. Aliye juu mngojee chini
C. Akili nyingi huondoa maarifa
D. Mtaka cha mvunguni sharti ainame

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kutoka 41-50

Watu zaidi ya kumi walipoteza maisha yao barabarani katika eneo la Salgaa kwenye barabara ya Nakuru-Eldor Eneo hili mara nyingi huwa na ukungu na hata utelezi barabarani. Salgaa huwa panakumbukwa kwa mkasa wa miaka zai ya miwili iliyopita ambapo zaidi ya watu mia moja walichomeka wakijaribu kuchota mafuta.

Lori la kubeba mafuta lilipinduka mahali hapo na yamkini **wakazi** waliiona kama njia rahisi ya kupata mafuta kutumia au hata kuuza. Cha msingi ni kuwa Salgaa ni eneo hatari ambalo madereva wanapaswa kuwa waangali wanapokaribia.

Ajali hiyo ilihusisha matatu na basi **imejiri** wakati serikali inapoendelea kutekeleza sheria ya trafiki iliyofanyiw marekebisho. Ingawa hapo awali waamiliki wa magari ya usafiri wa umma walipinga. Sheria hizo zilizoanza kutumika rasm Disemba mosi, ni dhahiri kuwa zinahitajika mno ili kukabiliana na vifo zaidi vya wananchi.

Isitoshe kumekuwa na kampeni nyingi za kuhamasisha watu kuhusu umuhimu wa usalama barabarani. Idara ya trafi ilituonyesha kuwa tulifanya vyema na kudhibiti ajali hizo kiwango kikubwa.

Lakini inaonekana wapo madereva wachache wazembe wanaendelea kuendesha magari kwa kasi bila kujali maish na usalama wa abiria wanaowabeba. Tunawahimiza wenye matatu na mabasi na hata madereva na abiria watambu kwamba kila mmoja ana wajibu wa kuzuia ajali.

Wakati huu kila mtu anatakiwa kuwa mwangalifu. Waswalihili husema 'kawia ufike.' Si lazima mtu ajifinyilie katik gari linaloendeshwa kwa kasi isiyoweza kudhibitiwa wakati chochote kinapotokea.

Maafisa wa trafiki nao wanapaswa 'kizidisha doria' kwenye barabara na kuwafikisha mahakamani mara moj watakaopatikana wakivunja sheria. Vifo hivi vya kiholela sharti vizuiwe.

41. Watu zaidi ya kumi walipoteza maisha yao barabarani, kwa hivyo:-
   A. walipiga ndoo teke
   B. walikata amri
   C. walikata kauli
   D. walisafiri ahera
42. Ukungu ni:
   A. moshi mweupe uliosababisha kutoona vizuri
   B. moshi mweusi unaoleta madhara
   C. vumbi jingi linalokosesha madereva kuona
   D. kali ya barabara kuwa telezi
43. Mkasa uliosababisha watu kuchomeka ulihusisha:
   A. watu kuuza mafuta
   B. watu kuchota mafuta kisha wakachomeka
   C. watu kufa baada ya lori kupinduka
   D. watu kufurahia kuchota mafuta
44. Neno wakazi kama lilivyotumika lina maana:
   A. watu wanaofanya kazi
   B. watu wanaofanya mambo kwa haraka
   C. wageni wa mahali fulani
   D. watu wanaoishi mahali fulani
45. Mambo yanayohusu magari ya umma na usafiri yapo chini ya wizara gani?
   A. Wizara ya maji
   B. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Ustawishaji wa maeneo ya Miji
   C. Wizara ya Usafiri na Miundomsingi
   D. Wizara ya ulinzi
46. Kwenye kufungu, kampeni zilizofanywa ni za:
   A. kueleza watu umuhimu usalama barabarani
   B. eneo la hatari Salagaa
   C. wamiliki wa magari ya umma
   D. ajali iliyohusisha watu kumi walioaga dunia
47. Kulingana na mwandishi iwapo gari limejaa kama abiria unapaswa kufanya nini
   A. panda gali lile chelewa utapata mwana si wako
   B. subiri jingine, subira huvuta heri
   C. msukume mwenzako na utahadhari kabla ya hatari
   D. panda gari lile mradi uyajali maisha yako
48. Madereva wamehimizwa waendeshe magari kwa kasi wanayoweza kudhibiti la sivyo yote haya yanaweza kutokea ila:
   A. vifo vya wasafiri
   B. gari kupoteza mwelekeo
   C. kupigana dafrao na gari jingine
   D. abiria kumwona dereva kuwa bingwa kwa kuendesha kasi
49. Polisi wamehimizwa 'kuzidisha doria.' Huku ni kusema nini?
   A. Kuwa waangalifu zaidi
   B. Kuwakamata madereva zaidi
   C. Kuwafikisha watu wengi zaidi mahakamani
   D. Kuweka vidhibiti mwendo zaidi
50. Mada ifaayo zaidi makala haya ni:
   A. Usalama barabarani
   B. uvunjaji sheria barabarani
   C. Ajali barabarani
   D. Kutekeleza sheria barabarani

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27